

# Salamu kutoka THAILAND!


Jifunze kuhusu watoto wa Baba wa Mbinguni ulimwenguni kote.



SHEREHE ZA SONGKRAN

Thailand ni nchi iliyopo Kusini Mashariki mwa Asia. Takribani watu milioni 72 wanaishi huko.

Watu wa Thailand husherehekea mwaka mpya wao kwa mchezo mkubwa ulimwenguni wa kupigana kwa maji. Wanarushiana maji ili kukumbuka kuosha mambo mabaya. Sherehe hudumu kwa siku tatu!



MASOKO YANAYOELEA

Nchini Thailand, watu huweza kufanya manunuzi kwenye mashua za mtoni, kama vile maduka madogo yanayoelea. Mito ni njia mojawapo ya kusafiri kuzunguka mji mkuu. Majengo mengi yapo juu ya nguzo ili yawe juu ya maji.



Hekalu la Pango la Chui-milia ni hekalu la Kibudha ambapo watu wengi huabudu na kusali. Ili kulifikia, lazima upande ngazi 1,260 kuelekea juu mlimani. Kuna alama za nyayo za chuimilia ndani ya pango!


PANGO LA CHUIMILIA



SHUGHULI

## Mkia Uliogongwa na Nyoka

Chagua mtu mmoja awe nyoka wa 1 na mwingine nyoka wa 2. Wengine wote wanasimama nyuma ya nyoka wa 1 na kumshikilia mtu aliye mbele yao. Nyoka wa 2 anajaribu kumpita nyoka wa 1 na kumfanya mtu wa mwisho kwenye mstari aachilie. Yeyote anayeachilia anatoka mchezoni!



MAELEZO YA UPISHI

## Som Tam

Saladi ya papai la kijani ni maelezo maarufu ya upishi nchini Thailand. Hapa ni toleo unaloweza kujaribu!

1. Ndani ya bakuli kubwa, changanya **kijiko 1 ½ cha sukari ya nazi (au sukari ya kahawia), kijiko 1 ½ cha sosi ya samaki (au soy sosi), na vijiko 2 vya maji ya ndimu**. Koroga mpaka sukari iyeyuke.
2. Saga **mbegu 2 za kitunguu saumu na pilipili nyekundu 1 au zaidi**. Katakata **maharage 3 ya kijani**. Kata **nyanya 1** katika umbo la kabari.
3. Menya **papai moja la kijani (au matufaha 3 ya kijani)**. Saga au kata katika vipande vidogo vidogo.
4. Ongeza kila kitu kwenye bakuli na changanya.



LUGHA

Kithai ndiyo lugha rasmi ya nchi. Alfabeti za Kithai zina herufi 72.

Kwa Kithai, unaweza kumkaribisha rafiki kwa kusema, "kin khao reu yang."

Ina maana, "Je, ume-shakula?"

Shukrani kwa Familia ya Pawarisa kwa kushiriki maelezo haya ya upishi!